

Kampuni yazindua ukumbi wa kisasa kusaidia vijana kibiashara

KAMPUNI ya Kikao64 imefungua ukumbi wa kisasa unaolenga kuwapa fursa vijana mjini Eldoret, Kaunti ya Uasin Gishu, kujistawisha kibiashara na kukuza vipaji vyao.

Kampuni hiyo inasema kuwa itawezesha wafanyabiashara wadogo, wanahabari, wasanii na makundi mengineyo, kupata afisi za kufanyia shughuli zao kwa kutumia teknolojia.

Gavana wa Uasin Gishu aliyekuwa akizungumza wakati wa hafla ya ufunguzi wa ukumbi huo ulio na inteneti na vifaa vinginevyo vya kiasasa, alisema kuwa ukumbi huo utawezesha vijana kujikwamua kimapato.

“Ukumbi huu wa Kikao64 utawezesha vijana kujistawisha kibiashara na serikali ya kaunti itahakikisha kwamba inaweka mazingira mwafaka ya kufanyia biashara,” akasema Gavana Mandago.

Kupitia mradi huo, wateja wataweza kukodisha afisi iliyowekewa inteneti, viti, meza na vifaa vinginevyo vya kisasa kwa bei nafuu. Wateja watumia mtandao kukodisha eneo la kufanyia kazi kwa muda wa siku moja, wiki au mwezi mmoja.

Na Leonard Onyango